

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA



MWONGOZO KWA WASAFIRI NA. 15 WA TAREHE 21 JANUARI 2025 KUFUATIA MLIPUKO WA UGONJWA WA MARBURG

Mnamo tarehe 20 Januari 2025, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) ilitangaza mlipuko wa Ugonjwa wa Virusi vya Marburg (MVD) ulioathiri Wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera, Kaskazini Magharibi mwa nchi ulio umbali wa kilomita 1,450 kutoka Dar es Salaam na kilomita 1,068 kutoka Arusha. Kufuatia mlipuko huu, Serikali ya JMT imeimarisha hatua za kudhibiti mlipuko huo ili kuzuia kusambaa ndani na nje ya nchi kulingana na Kanuni za Afya za Kimataifa za mwaka 2005. Serikali imeandaa Mwongozo Na. 15 wa tarehe 21 Januari 2025 kwa wasafiri kuhusiana na ugonjwa huu utakaoanza kutumika mara moja ili kutekeleza hatua madhubuti zinazohusiana na safari za ndani na za kimataifa kama ifuatavyo:

1. Wasafiri wote kutoka Mkoa wa Kagera wanatakiwa kujaza kwa uaminifu fomu ya ufuatiliaji wa hali ya afya ya wasafiri iliyopo katika mtandao kwa anuani <https://afyamsafiri.moh.go.tz>.
2. Watu wote waliokuwa karibu na mgonjwa wa Marburg ambao wanafuatiwa na wataalamu wa afya hawaruhusiwi kusafiri mpaka watakapomaliza kipindi cha ufuatiliaji na kuruhusiwa na mamlaka za afya.
3. Katika kila Mpaka wa nchi (viwanja vya ndege, mipaka ya nchi kavu au bandari), wasafiri wote watapimwa joto la mwili na watakabainika kuwa na homa watafanyiwa uchunguzi wa kina na Mamlaka za afya Mipakani.
4. Elimu, utoaji wa taarifa mapema na ushauri wa afya kuhusu kuripoti dalili zozote za ugonjwa wa Marburg vitatolewa kwa wasafiri wote mipakani au kwa kupitia namba ya bure ya simu **199**. Wale watakaonesha dalili hizo watafanyiwa uchunguzi wa kina na kupatiwa matibabu katika vituo vya huduma za afya.
5. Wasafiri wote na wafanyakazi mipakani wanapaswa kuzingatia hatua za kujikinga na kudhibiti maambukizi kama vile kunawa mikono au kutumia vitakasa mikono (sanitizer), kuepuka misongamano inayosababisha kugusana, na kuripoti dalili yoyote kwa kutumia namba ya bure ya simu **199**.
6. Wasimamizi wote wa vyombo vya usafiri na madereva wanapaswa kufuata hatua za uchunguzi Mipakani, ikijumuisha uchunguzi wa afya, ukaguzi wa usafi wa vyombo vya usafiri, kunawa mikono, matumizi ya vitakasa mikono, na kutoa taarifa mara moja kuhusu msafiri yeyote mwenye dalili zozote kwa mamlaka za afya mipakani.

NB: Mwongozo huu wa wasafiri utakuwa ukihuishwa mara kwa mara kadri itakavyohitajika.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Seif A. Shekaraghe'.

Dkt. Seif A. Shekaraghe

KATIBU MKUU